UCHAGUZI

Jarida la Tume ya Taifa ya Uchaguzi Toleo Na. 16 Oktoba, 2023

Muungano wa Tume za Uchaguzi Duniani wapongezwa

Tahamu Tume

Njia za Utoaji Elimu ya Mpiga Kura

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikitekeleza mkakati wa kutoa Elimu ya Mpiga Kura endelevu kwa kutumia njia zifuatazo;

(I)Mikusanyiko rasmi ya watu: Tume inatumia maonyesho mbalimbali kama vile Sabasaba, Nanenane, Mikutano ya Serikali za Mitaa (ALAT) na wiki ya vijana kwa kutoa Elimu ya mpiga Kura ana kwa ana au kuwapatia vijitabu na vipeperushi vyenye kuonesha hatua mbalimbali za mchakato wa uchaguzi;

(ii)Mikutano na wadau: Tume hufanya mikutano na wadau mbalimbali ikiwa ni njia ya kutoa taarifa na elimu ya mpiga kura. Mikutano hiyo imekuwa ikifanyika kabla ya kuanza mazoezi ya mchakato wa uchaguzi.

(iii)Vipindi vya Redio na Televisheni: Tume inaandaa na kutekeleza programu ya kushiriki katika vipindi mbalimbali vya redio na runinga ili kuweza kuwaelimisha wananchi kuhusu sheria,kanuni na maelekezo.

(iv)Makala za magazeti: Tume huandaa makala zinazohusu masuala ya Uchaguzi na kuzichapisha katika magazeti mbalimbali nchini kwa lengo la kutoa habari na kuelimisha umma kuhusu Sheria, kanuni na taratibu za uendeshaji Uchaguzi.

(v)Mitandao ya Kijamii: Tume imekuwa ikitumia mitandao ya kijamii katika kutoa habari za kuelimisha na kuhabarisha.

(vi)Vijitabu, vijarida na vipeperushi: Tume imekuwa ikiandaa vijitabu na vijarida mbalimbali ambavyo huvigawa kwa wananchi bure.

(vii)Sanaa: Tume imekuwa ikitumia nyimbo na michezo ya kuigiza ambayo huandaliwa kwa kushirikiana na wasanii mbalimbali. Nyimbo hizo na michezo hutumika katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

(viii)Gari la Matangazo: Tume hutumia gari lake la matangazo ambalo hupita katika maeneo mbalimbali yenye mikusanyiko ya watu kama vile stendi, sokoni, minadani na shuleni ili kutoa Elimu ya Mpiga kura ana kwa ana.

Muungano wa Tume za Uchaguzi Duniani waponzezwa

Na Mwandishi wetu

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imeupongeza Muungano wa Tume za Uchaguzi Duniani (The Association of World Election Bodies A-WEB) kwa kutimiza miaka 10 tangu kuanzishwa kwake.

Aidha Tume imesema itaendelea kutoa ushirikiano kwa Sekretarieti ya A-WEB kwenye kila nyanja muhimu za mashirikiano na inaamini kuwa maadhimisho ya miaka 10 ya A-WEB yatazidi kuimarisha muungano huo.

Katika salamu zake za pongezi alizozitoa kwa Katibu Mkuu wa muungano huo, Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele amesema ushirikiano wa Tume na muungano huo katika kipindi cha miaka 10 umekuwa na manufaa makubwa katika kukuza ujuzi na uzoefu kwa watumishi wake.

Amesema kupitia ushirikiano huo, baadhi ya watumishi wa Tume walipata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ambayo yalitolewa kwa njia ya mtandao, lakini pia watumishi hao walipata fursa ya kushiriki katika misheni za utazamaji wa uchaguzi.

“Mafunzo haya yametuongezea ujuzi na maarifa mapya katika kuendesha michakato yetu ya ndani na pia kuona ni kwa namna gani tunaweza kushirikiana na wadau wetu wakuu kama vile vyama vya siasa, wagombea, wapiga kura, umma kwa ujumla na vyombo vya habari” amesema Jaji Mwambegele.

Mwenyekiti huyo wa Tume ameongeza kuwa tangu kuanzishwa kwake tarehe 13 Januari, 1993 Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wa kikanda na kimataifa, mashirika na vyama vya siasa kama vile A-WEB kwa lengo la kubadilishana uzoefu kuhusu michakato na taratibu za uchaguzi.

Jaji Mwambegele amekumbusha kuwa tarehe 14 Oktoba 2013, ilikuwa tarehe muhimu na isiyoweza kusahaulika kwa Tume kwani ndio siku NEC ilipojiunga na Muungano huo

“Tangu wakati huo, hatujutii kuwa sehemu ya muungano huu imara na ambao una viwango tofauti vya matarajio ya usimamizi wa uchaguzi kutoka kwa tume wanachama za uchaguzi” amesema na kuongeza:

“Kupitia muungano huu,

tunajifunza, tunabadilishana uzoefu na kukuza fikra zetu kuhusu michakato na taratibu za uchaguzi ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia yanayotokea ulimwenguni.”

Aidha, Mwenyekiti wa Tume amemshukuru na kumpongeza Katibu Mkuu wa muungano wa A-WEB na sekretarieti nzima kwa kuratibu kongamano la maadhimisho linaloashiria ukomavu wa muungano huo katika umri wake mdogo wa miaka 10.

“Ni matumaini yangu kwamba muungano huu utaendelea kuimarika na kutoa fursa zaidi ambazo zitakuwa na manufaa kwa wanachama wote na tena natumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Katibu Mkuu na timu yake juu ya kile kilichofanyika,” amesema.

Mwenyekiti wa Tume amesema kutokana na A-WEB kujenga utamaduni wa kufanya tafiti na kutoa machapisho yake ya kila mwezi upatikanaji wa taarifa kwa wanachama umerahisishwa ambapo tume hizo hupata fursa ya kufahamu nini kinatokea katika A-WEB na kwa wanachama wake kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele.

TAHARIRI

Kundi la watu wenye ulemavu ni miongoni mwa makundi katika jamii yetu ambayo ushiriki wake katika michakato mbalimbali ya kijamii ikiwemo ya uchaguzi ni mdogo kutokana na kundi hili kukosa nafasi ya kupata taarifa sahihi na za kutosha kuhusu michakato hiyo.

Hali hii imechangiwa kwa kiasi kikubwa na mila potofu katika baadhi ya jamii ambazo haziwapi nafasi ya kushiriki katika shughuli za kiuchumi, kijamii na kisiasa.

Matokeo yake kundi hili linakosa taarifa sahihi na za kutosha kuhusu michakato mbalimbali ya uchaguzi ikiwemo kutofahamu uwepo wa mahitaji au vifaa mbalimbali ambavyo vinaliwezesha kundi hili kushiriki kwenye michakato ya uchaguzi kwa njia iliyo rahisi.

Jamii yetu inapaswa kutambua kuwa ushiriki wa watu wenye ulemavu katika siasa hususani katika michakato ya uchaguzi utaiwezesha jamii hiyo kutambua haki, wajibu na umuhimu wa kushiriki katika kupiga kura na pia haki ya kuwania nafasi mbalimbali za uongozi ili waweze nao kuchaguliwa kwenye michakato mbalimbali ya uchaguzi.

Hivyo, tunapenda kutoa rai kwa baadhi ya jamii zetu za kitanzania kuachana na mila potofu za kutowapa nafasi watu wenye ulemavu nafasi ya kushiriki kwenye michakato ya uchaguzi ili jamii hiyo iweze kutimiza haki yao ya kupiga na kupigiwa kura.

Kadhalika, tunavisihi vyama vya siasa vitoe nafasi kwa jamii ya watu wenye ulemavu kushiriki kugombea katika chaguzi mbalimbali za kidemokrasia na pia wawape nafasi ya kuwania nafasi za uongozi katika vyama vyao.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikishirikiana na Wadau mbalimbali wa Uchaguzi wakiwemo watu wenye ulemavu katika kuhakikisha kila mwananchi anapata Elimu ya Mpiga Kura.

Kupitia elimu ya mpiga kura, Tume inahakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata taarifa sahihi na za kutosha kuhusu uwepo wa Jalada la nukta nundu (tactile ballot folder) kwenye vituo, kufahamu matumizi ya kituturi kwamba kinamwezesha mwenye ulemavu wa viungo kupiga kura, kupewa kipaumbele wafikapo vituoni na pia kuruhusiwa kwenda na wasaidizi wao kituoni ili waweze kupiga kura kwa urahisi.

NEC yateua Mbunge Viti Maalum

Na Mwandishi wetu

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imemteua Bi. Aziza Ally Sleyum kuwa Mbunge wa Viti Maalum katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM).

Uteuzi huo umefanyika kwa kuzingatia matakwa ya ibara ya 78(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 ikisomwa pamoja na kifungu cha 86A (6) na (8) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, Sura ya 343 ambayo inaeleza utaratibu wa kufuatwa kuhusu uteuzi wa Wabunge wa Viti Maalum.

Taarifa ya Mkurugenzi wa Uchaguzi Bw. Ramadhan Kailima imeeleza uteuzi huo umefanyika baada ya Tume kupokea barua kutoka kwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiitaarifu Tume kuhusu kuwepo nafasi ya wazi ya ubunge kufuatia kujiuzulu kwa aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Bahati Ndingo.

Mhe. Ndingo alijiuzulu nafasi hiyo ya ubunge Agosti 17 mwaka huu ili kuwania ubunge katika Jimbo la Mbarali, baada ya aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo Francis Mtega kufariki dunia Julai Mosi, mwaka.

Watumishi NEC waomboleza kifo cha mtumishi mwenzao

Na Mwandishi wetu

Watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakiongozwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi Bw. Ramadhani Kailima waliungana na mamia ya wakazi wa jiji la Dar es salaam katika mazishi ya aliyekuwa mtumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Marehemu Numpele Caroline Mulungu ambaye alifariki dunia tarehe 16/09/2023 katika Hospitali ya Agha Khan.

Ibada ya mazishi ya Marehemu Numpele ilifanyika tarehe 19/09/2023 katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania KKKT Usharika wa Boko, Dar Es Salaam na kufuatiwa na mazishi yake ambayo yalifanyika katika makaburi ya Kondo yaliyopo Kunduchi jijini Dar es salaam.

Mazishi ya Numpele yaligubikwa na majonzi, vilio, na huzuni kutoka kwa ndugu, jamaa na marafiki pamoja na watumishi wenzake wa Tume ambapo Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Bw. Deodatus Mwiliko alimwelezea marehemu Numpele kuwa alikuwa mchapa kazi, hodari na mwenye kufanya kazi kwa ushirikiano na watumishi wenzake wa idara na taasisi kwa ujumla.

“Kwa niaba ya Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, tunawapa pole mume wa marehemu, wazazi wa marehemu, ndugu wa marehemu,

watumishi wote wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, jamaa, marafiki na wafiwa wote," amesema.

Mwiliko amesema kuwa hadi umauti unamkuta marehemu alikuwa anafanya kazi katika ofisi za Tume kama Afisa TEHAMA Mkuu tangu mwaka 2015 akitokea Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.

Marehemu alifanya kazi katika Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi kama Afisa TEHAMA kati ya mwaka 2009 hadi 2015 na aliajiriwa na Shirika la Posta Tanzania kwa cheo cha Afisa TEHAMA mnamo mwaka 2001 na kuendelea kufanya kazi katika ofisi hiyo hadi mwaka 2008.

Mkurugenzi wa Uchaguzi Bw.Ramadhan Kailima akiweka Shada la Maua kwenye kaburi la Bi.Numpele Mulungu.

Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti na Watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakiwa nyumbani kwa Marehemu Bi.Numpele Mulungu, Mbweni jijini Dar es Salaam.

Jukwaa la ECF - SADC lashiriki kutazama Uchaguzi Eswatini

Na Mwandishi wetu

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) ilikuwa ni miongoni mwa Tume tisa wanachama zilizo chini ya mwamvuli wa Jukwaa la Tume za Uchaguzi za Kusini mwa Afrika (ECF-SADC) ambazo zilishiriki katika misheni ya kutazama uchaguzi mkuu nchini Eswatini kuanzia tarehe 21 septemba hadi 03 oktoba, 2023.

Lengo kuu la misheni hiyo lilikuwa ni kutazama namna Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Eswatini (Election and Boundaries Commission) iliyokuwa imejiandaa kusimamia na kuendesha uchaguzi Mkuu wa nchi hiyo ambao ulifanyika tarehe 29 Septemba, 2023.

Katika misheni hiyo, Ujumbe wa ECF - SADC uliongozwa na Bibi Wendy Didon, ambaye ni Kamishna kutoka Tume ya Uchaguzi ya Shelisheli, huku Tume ya Taifa ya Uchaguzi iliwakilishwa na Mwenyekiti wa Tume hiyo Mhe. Jaji Rufaa Jacobs Mwambegele pamoja na Mkurugenzi wa Idara ya Usimamizi wa Uchaguzi Bw. Grayson Orcado. Tume nyingine wanachama wa ECF - SADC zilizoshiriki katika misheni hiyo ni pamoja na Malawi, Angola, Msumbiji, Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Afrika ya Kusini, Shelisheli na Namibia.

Ujumbe huo wa ECF SADC ulipata pia fursa ya kuangalia ni kwa namna gani nchi ya Ufalme wa Eswatini imejipanga kwa ajili ya kusimamia

na kuendesha Uchaguzi Mkuu ujao ikiwa ni pamoja na kuangalia zoezi la uandikishaji wa wapiga kura kwenye Daftari la Wapiga kura, ushirikishwaji wa wadau wa uchaguzi, Elimu ya mpiga kura na elimu ya uraia.

Jukwaa la Tume za Uchaguzi za nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika

(ECF-SADC) ni taasisi huru ambayo inajumuisha tume za uchaguzi 15 kutoka nchi 14 wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC).

Mbali na tume hizo tisa za uchaguzi zilizoshiriki kwenye misheni ya utazamaji nchini Eswatini, tume nyingine wanachama zinazounda Jukwaa la ECF-SADC ni pamoja na Tume za Uchaguzi za Zanzibar, Zambia, Zimbabwe, Eswatini, Lesotho na Mauritius.

Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi Mhe. Jaji (Rufaa) Jacobs Mwambegele wa sita kutoka kushoto, akiwa katika picha ya pamoja na wajumbe wengine wa misheni ya ECF-SADC katika Ofisi za Tume ya Uchaguzi na Mipaka ya Eswatini.

Jinsi Tume ya Taifa ya Uchaguzi inavyoweka mazingira wezeshi kwa Watu wenye Ulemavu

Na Mwandishi wetu

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali wa uchaguzi kama vile vyama vya siasa, wapiga kura, viongozi wa dini, vyombo vya habari, asasi za kiraia, wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Tume kupitia elimu ya mpiga kura hutoa kipaumbele kwa kundi la watu wenye ulemavu kwa sababu kwa kiasi fulani limekuwa likiachwa nyuma ukilinganisha na makundi mengine.

Tume imehakikisha kuwa watu wenye ulemavu wanapata taarifa sahihi na kwa wakati kuhusu mchakato wa uchaguzi.

Kadhalika Tume imeboresha zaidi njia ya kuwasiliana na watu wenye ulemavu wa kusikia kwa kutoa elimu ya mpiga kura kwa lugha ya alama.

Elimu itolewayo ni sawa na ile ambayo wadau wengine wa uchaguzi wanaipata kwa njia ya mazungumzo ya kawaida.

Mathalani, Tume huandaa video za Lugha ya Alama ambazo mtu mwenye uziwi anaweza kuziangalia na kuelewa. Video hizi tayari zimeanza kuwekwa katika kurasa za mitandao ya kijamii ya Tume.

Kuwepo kwa Jalada la nukta nundu kwenye vituo vya kupigia kura (tactile ballot folder), humsaidia mtu asiyeona kusoma namba ya chama ambacho anapenda kukipigia kura pasipo kumtegemea mtu mwingine.

Kadhalika, fursa imetolewa kwa mpiga kura mwenye ulemavu kwenda na mtu anayemwamini kutoka nyumbani kwake au katika familia yake ili akamsaidie kupiga kura kama ambavyo yeye amependekeza.

Aidha, Tume hutoa Elimu ya Mpiga Kura kila siku asubuhi katika kipindi cha magazetini ambacho hurushwa na NEC Online TV ambapo mtu asiyeona anaweza kusikiliza elimu hiyo ikitolewa kwa njia ya mazungumzo.

Pamoja na hayo Tume huratibu na kusimamia mikutano ya wadau wakiwemo watu wenye ulemavu kuhusu elimu ya mpiga kura ambapo hupata fursa ya kujadili changamoto zinazowakabili na kufahamu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya kuzingatiwa ili waweze kushiriki kikamilifu katika michakato ya uchaguzi.

Tume huzingatia pia mahitaji ya watu wenye ulemavu wa viungo (miguu) kwa kuandaa kifaa maalum cha faragha (kituturi) ambacho humwezesha mlemavu kupiga kura yake hata akiwa amekaa kwenye kiti mwendo.

Pia watu wenye ulemavu wanapofika kwenye vituo vya kuandikishia wapiga kura na vya kupigia kura, hupewa kipaumbele kwa kuwa na mstari wao tofauti na ule wa wapiga kura wengine ili kuwapunguzia adha ya kukaa muda mrefu kituoni.

Ikumbukwe kuwa ni haki na wajibu wa watu wenye ulemavu kushiriki kwenye uchaguzi ili kuchagua viongozi wanaowataka katika maeneo yao na wajibu wa Tume ni kuweka mazingira wezeshi.

Watumishi NEC wahimizwa kushiriki kwenye michezo.

Na Mwandishi wetu

Watumishi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) wamehimizwa kujenga utamaduni wa kufanya mazoezi mara kwa mara ili kujiweka sawa kiafya na pia waweze kushiriki kikamilifu katika mashindano mbalimbali yakiwemo Mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali na Mikoa (SHIMIWI).

Wito huo umetolewa tarehe 25 Oktoba, 2023 na Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo ya NEC Bw.Juvenali Kaiza, wakati akitoa tathmini ya ushiriki wa timu yake katika mashindano ya SHIMIWI yaliyomalizika hivi karibuni katika uwanja wa Samora uliopo mjini Iringa.

Amesema watumishi wa NEC sambamba na kutekeleza majukumu yao mbalimbali ya kiofisi, wanapaswa kutenga muda wao kushiriki kwenye michezo mbalimbali na kufanya mazoezi mara kwa mara ili waweze kuiweka miili yao vizuri na hivyo kuiwezesha timu ya NEC kushiriki kikamilifu katika mashindano mbalimbali yajayo.

Bw.Kaiza ameitaja michezo ambayo watumishi wa NEC wanaweza kushiriki ikiwa ni pamoja na mpira wa miguu, netiboli, riadha, na michezo ya jadi.

Akizungumzia ushiriki wa timu yake katika mashindano ya SHIMIWI mwaka huu, Bw.Kaiza amesema kuwa pamoja na kupeleka wachezaji katika michezo michache, lakini timu yake iliweza kufanya vizuri katika michezo ya jadi ambapo mchezaji wao Bi. Atonda Ikomba aling'ara katika mchezo wa karata na alifanikiwa kumtoa mchezaji kutoka timu ya Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST) kwa pointi 2-0, na katika hatua ya robo fainali NEC iliishinda ikulu kwa pointi 2-0.

Kwa upande wa michezo ya Jadi ya Bao na Draft, timu za wanaume na wanawake kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi ziliishia katika hatua ya makundi. Timu ya Bao kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikiwakilishwa na Bi. Christer Njovu na timu ya wanaume iliwakilishwa na Mussa Simba.

Mshindi wa mchezo wa Draft kwa upande wa wanaume ni timu kutoka Wizara ya Ujenzi, na mshindi wa mchezo wa Bao alitoka RAS Lindi.

Katika Mashindano ya 37 ya SHIMIWI kwa mwaka 2023, timu ya NEC haikufanikiwa kupeleka wachezaji katika michezo ya mpira wa miguu, netiboli, na michezo ya riadha kama vile mbio fupi, na mbio ndefu, na mbio za baiskeli.

Klabu ya Michezo ya NEC iliwakilishwa na wachezaji katika michezo ya kuvuta kamba, wanawake kwa wanaume, ambapo waliishia hatua ya 16 bora, mchezo wa jadi wa karata wanaume na wanawake na kuwa mshindi wa nne, huku wachezaji kutoka NEC katika michezo ya jadi ya Bao, Draft na mchezo wa riadha wa kurusha tufe waki-ishia katika hatua za makundi.

Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo ya Tume ya Taifa Uchaguzi, Mwalimu Juvennile Kaiza

Matukio katika Picha

Mwenyekiti wa Klabu ya Michezo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Mwalimu Juvenille Kaiza (Kushoto)akipokea mpira kutoka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, Bw. Leonard Tumua (Kulia) ikiwa ni ishara kumtakia heri Mwenyekiti huyo kuelekea michezo ya SHIMIWI. Katikati ni Mkurugenzi msaidizi Idara ya utawala na Rasilimali watu (Sehemu ya usimamizi wa Rasilimali watu)Bi.Hidaya Gwando.

Mtumishi wa Tume ya taifa ya Uchaguzi Bi.Atonda Ikomba akicheza karata dhidi ya mtumishi kutoka GST wakati wa michezo ya SHIMIWI mkoani Iringa.

Mtumishi wa Tume ya taifa ya Uchaguzi Bw.Salu Mdegela akicheza karata dhidi ya mtumishi kutoka wizara ya Viwanda wakati wa michezo ya SHIMIWI mkoani Iringa.

Timu ya Kamba wanawake kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi, wakivuta Kamba wakati wa mchezo dhidi Mahakama katika Mashindano ya SHIMIWI mkoani Iringa.

Timu ya Kamba kutoka Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikijiandaa kuvuta Kamba wakati wa mchezo wao dhidi ya Timu kutoka Ikulu wakati wa Mashindano ya SHIMIWI mkoani Iringa.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi
Makao Makuu Dodoma,
5 Barabara ya Uchaguzi,
41107 Njedengwa,
Uchaguzi House,
Anuani: S.L.P 358, Dodoma
Namba ya simu: +255 26 2962345-8
Nukushi: +255 26 2962348
Barua pepe: Uchaguzi@nec.go.tz

www.nec.go.tz tumeyauchaguzi_tanzania

Tume ya Uchaguzi-TZ Tume ya Uchaguzi-tz NEC online TV